

*Shairi lifuatalo limeandikwa na Mshairi Bakari Mwamboga wa Uholanzi, ambaye anatuasa katika uvumilivu, na kukabiliana na maisha ya kila siku, kujiepusha na shari, ikiwa pamoja na kuendesha maisha yaliyo jawa na busara na hekima.*

## **MOYO**

1. Moyo sema nami moyo, usiingie unyonge,  
Moyo silie kwa hayo, na kimya usijitenge,  
Moyo yasemwayo siyo, waja wasikuvononge,  
Moyo wangu ewe moyo, subira usiipinge
2. Moyo wangu wa imani, sitiririke machozi,  
Moyo kumbuka manani, ayaona maonezi,  
Moyo ungefanywa duni, na kusemwa kwa ufyози,  
Moyo ngojea thamani, ya kupewa na mwenyezi
3. Moyo wangu sikereke, kuwapa waja faida,  
Moyo usipaparike, unapofikwa na shida,  
Moyo usisikitike, kila jambo lina mda,  
Moyo wala sitamke, kaa kimya kawaida
4. Moyo mengi vumilia, wanayo kutenda waja,  
Moyo wajibu tulia, waachie zao hoja,  
Moyo wangu zingatia, fahamu mambo kangaja,  
Moyo yasemwayo chuja, jitahadhari sikia
5. Moyo ujitaarishe, ya leo siyo ya kale,  
Moyo hili jikumbushe, ufanyalo ona mbele,  
Moyo sijiteremshe, heshima si makelele,  
Moyo wangu vile vile, penye chuki jiepushe
6. Moyo mwenzangu ni wewe, usiniwache mkono,  
Moyo mabaya yasiwe, jiepushe na sonono,  
Moyo wangu jikombowe, ishi kwa mema mifano,  
Moyo sifate maneno, hili na wewe ujuwe
7. Moyo jasho la tiriri, latiririka kwa wingi,  
Moyo uwe mjasiri, tujijengee msingi,  
Moyo wangu tafakuri, kuishi kuona mengi,  
Moyo wangu sikutengi, nakuomba tahadhari
8. Moyo moyo wangu ishi, maisha ni taratibu,  
Moyo toa tashuwishi, siku za raha na tabu,  
Moyo dhiki haziishi, vibaya kujiadhibu,  
Moyo uwe na adabu, uwe hujitamanishi
9. Moyo nasema tamati, hapa nafunga uneni,  
Moyo napanga wakati, manufaa ya mbeleni,  
Moyo ona tofauti, akhera na duniani,  
Moyo mjuwe Manani, uepuke tasiliti

***B. Mwamboga  
Holland  
01.04.03***